**SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Matumizi.

3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA KWA WAKALA**

4. Kuanzishwa kwa Wakala.

5. Muhuri na nembo ya Wakala.

6 Kazi za Wakala.

7. Uwezo wa Wakala.

**SEHEMU YA TATU**
**UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA WAKALA**

8. Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

9. Sifa za Mwenyekiti.

10. Makamu Mwenyekiti.

11. Katibu wa Bodi.

12. Kazi za Bodi.

13. Uwezo wa Bodi.

14. Posho za wajumbe.

15. Mwenendo wa Bodi.

16. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

17. Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

18. Idara, divisheni na vitengo.

19. Wafanyakazi wa Wakala.

20. Kuanzishwa kwa Kamati ya Uongozi.

21. Kazi za Kamati ya Uongozi.

**SEHEMU YA NNE**
**MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR**

22. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

23. Uendeshaji na usimamizi wa Mfuko.

24. Vyanzo vya Mfuko.

25. Malengo ya Mfuko.

26. Ukaguzi wa Mfuko.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA FEDHA**

27. Vyanzo vya fedha.

28. Bajeti ya Wakala.

29. Hesabu na ukaguzi.

## SEHEMU YA SITA
## USAJILI WA MJASIRIAMALI NA MFANYABIASHARA

30. Maombi na taratibu za usajili.

31. Daftari la kumbukumbu.

32. Sifa za kusajiliwa.

33. Cheti cha usajili.

34. Athari ya usajili.

35. Kufuta Cheti cha Usajili.

36. Athari ya kufutwa kwa Cheti cha Usajili.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

37. Makosa na adhabu.

38. Adhabu ya jumla.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

39. Thamani ya Wadau wa Ndani na Jukumu la Ushirikishaji Jamii.

40. Rufaa.

41. Kanuni.

42. Kufuta na kubakiza.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 2 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

.........21 Machi........., **2022**

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi.

**2.** Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, Sheria hii itatumika kwa masuala yote yanayohusiana na uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara waliosajiliwa Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ulioanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Muombaji" maana yake ni mjasiriamali au mfanyabiashara anayeomba kwa Wakala kupatiwa huduma za uwezeshaji kiuchumi;

"Mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote ambaye tayari ameshajihusisha na shughuli halali za kibiashara;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mkopo" maana yake ni fedha au vifaa vilivyokopeshwa kwa mjasiriamali au mfanyabiashara ili kumuwezesha kuanza au kuendeleza shughuli zake za kiuchumi na ambavyo vitahitajika kulipwa;

"Shughuli za kiuchumi" maana yake ni shughuli zozote halali na zinazokubalika katika mazingira ya Zanzibar ikiwa rasmi ama si rasmi zenye lengo la kujipatia kipato na kuimarisha hali ya maisha ya mjasiriamali au mfanyabiashara;

"Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi" maana yake ni hatua zote ambazo zinajumuisha uwezeshaji kifedha, ujuzi, mafunzo, miundombinu, ushauri au kuunganishwa na masoko ambazo zitamuwezesha mjasiriamali au mfanyabiashara kufanya shughuli za kiuchumi kwa mafanikio;

"Programu ya elimu" maana yake ni shughuli zote zinazohusiana na utoaji wa elimu na uzoefu kwa mjasiriamali au mfanyabiashara itakayomuwezesha kufanya shughuli zake za kiuchumi;

"Mjasiriamali" maana yake ni mtu binafsi au makundi yaliyosajiliwa ambayo yapo tayari kukabiliana na changamoto katika shughuli za uwezeshaji kiuchumi kwa madhumuni ya kupata faida za kiuchumi zinazotarajiwa;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala anayeteuliwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar unaoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Taasisi ya kifedha" maana yake ni taasisi inayojihusisha na miamala ya kifedha au fedha;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Masoko" maana yake ni hatua zote ambazo zinawezesha ubadilishaji wa bidhaa au huduma kwa kitu chenye thamani;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Daftari la kumbukumbu" maana yake ni daftari la kumbukumbu lilioanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mafunzo" maana yake ni utoaji wa ujuzi kwa mjasiriamali au mfanyabiashara ili kumuwezesha kufanya shughuli zake za kiuchumi kwa ufanisi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA

Kuanzishwa kwa Wakala.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Wakala utakaojulikana kama Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na kwa ufupisho wake ZEEA.

(2) Wakala itakuwa ni chombo cha Serikali kisichojitegemea kikamilifu na kwa idhini ya Waziri na kwa kutumia jina lake itakuwa na uwezo wa:

(a) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(b) kupata, kununua, kumiliki na kuondosha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kukopa au kukopesha fedha; na

(d) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo Wakala kwa nafsi yake anaweza kulitekeleza kwa mujibu wa sheria.

Muhuri na nembo ya Wakala

**5.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Wakala katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya jina fupi, muhuri na nembo ya Wakala katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Wakala utawekwa muhuri wa Wakala na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Wakala.

**6.** Wakala utakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kupanga na kuandaa bajeti;

(b) kutoa ushauri kwa Serikali, taasisi za umma na binafsi kwa mambo mahsusi na njia zinazolenga katika kushajiisha uwezeshaji kiuchumi Zanzibar;

(c) kufanya au kuratibu programu za mafunzo na elimu, huduma za ushauri elekezi, masoko na utoaji wa mitaji kwa wajasiriamali au wafanyabiashara;

(d) kushirikiana na kuingia katika ubia na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya utekelezaji bora wa mamlaka yake;

(e) kuwatambua, kuwahakiki na kuwaunganisha wajasiriamali na wafanyabiashara na taasisi za kifedha;

(f) kushauri juu ya uanzishwaji na uimarishwaji wa mtu binafsi au makundi ya jamii, ubia au mashirikiano katika shughuli za kiuchumi;

(g) kushajiisha ufanyaji wa tafiti juu ya shughuli za kiuchumi na kuimarisha mahusiano na taasisi za utafiti;

(h) kuanzisha na kuendeleza Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa wa shughuli za Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi katika sekta mbali mbali na kuwezesha usambazaji wa taarifa;

(i) kupendekeza juu ya namna na hatua za kuchukua zitakazohakikisha upatikanaji wa huduma za mikopo;

(j) kuchunguza au kukagua nyaraka zinazohusiana na mwenendo wa mjasiriamali au mfanyabiashara;

(k) kumtambua mjasiriamali au mfanyabiashara mwenye sifa kwa madhumuni ya kumuingiza katika programu za uwezeshaji;

(l) kushajiisha kuweka akiba na uwekezaji;

(m) kuendeleza mawazo ya biashara;

(n) kutambua na kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa na huduma zinazotolewa na mjasiriamali au mfanyabiashara;

(o) kuwezesha utoaji wa mikopo na kuhakikisha unarudishwa kwa wakati;

(p) kumuunganisha mjasiriamali au mfanyabiashara na vituo vya mafunzo ya amali;

(q) kuwaleta pamoja wajasiriamali au wafanyabiashara wenye maslahi yanayofanana katika shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kuunda kongano;

(r) kumsajili au kumfuta mjasiriamali au mfanyabiashara katika daftari la kumbukumbu;

(s) kutafuta rasilimali kutoka katika vyanzo vya ndani na nje; na

(t) kufanya kazi nyengine yoyote itakayoona inafaa.

Uwezo wa Wakala.

**7.** Wakala utakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuweka taratibu za usajili;

(b) kuandaa miongozo ya utekelezaji wa programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi na sera;

(c) kuweka dhamana ya mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara inayotolewa na taasisi za fedha zilizo na makubaliano na Serikali; na

(d) kusimamia utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA WAKALA

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

**8.-**(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji ambaye ni mjumbe anayeingia kwa nafasi yake;

(c) Mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na Uwezeshaji;

(d) Mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na Fedha; na

(e) Wajumbe wanne kutoka sekta tofauti.

(2) Wajumbe chini ya aya ya (c), (d) na (e) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kuzingatia uzoefu, ujuzi, weledi na jinsia.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika Chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi angalau miaka mitano na kiwango cha juu cha weledi wa kusimamia kwa ufanisi shughuli za vyombo vya umma au binafsi; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Makamu Mwenyekiti.

**10.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

**11.**-(1) Bodi itamteua mtumishi wa umma mwenye sifa zifuatazo kuwa Katibu wa Bodi:

(a) awe na angalau shahada ya kwanza katika Chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) awe muadilifu wa hali ya juu;

(c) awe na uwezo wa kutumia vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na

(d) awe anaweza kutunza siri.

(2) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na:

(a) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(b) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(d) atatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(e) atafanya kazi nyengine zozote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**12.** Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia uendeshaji wa jumla wa Wakala;

(b) kuidhinisha ada na tozo zitakazotozwa kwa huduma zinazotolewa na Wakala;

(c) kumshauri Waziri juu ya mambo yanayohusiana na maendeleo na uendeshaji wa Wakala;

(d) kuhakikisha utekelezaji mzuri wa sera zilizoidhinishwa na Waziri ambazo zinasimamia uendeshaji wa Wakala;

(e) kuratibu, kusimamia na kuidhinisha utekelezaji wa mpango mkakati, mpango wa utekelezaji wa mwaka, bajeti, ripoti za utekelezaji, sera na miongozo ya Wakala;

(f) kuidhinisha ripoti za Wakala zitakazowasilishwa kwa Waziri;

(g) kuishauri Serikali juu ya masuala yanayohusiana na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(h) kuuwezesha Mfuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(i) kufuatilia utekelezaji wa uendeshaji wa Mfuko;

(j) kuhakikisha kwamba Mfuko ni endelevu kwa kubuni vyanzo vyengine vya fedha;

(k) kubuni njia bora za kuimarisha ufanisi katika utoaji na urejeshaji wa mkopo;

(l) kutathmini maendeleo ya Mfuko na kuweka kumbukumbu za mifano bora ili iweze kutumika kushajiisha na kuimarisha shughuli za Mfuko;

(m) kuidhinisha mikopo yote iliyowasilishwa mbele yake; na

(n) kutekeleza kazi nyengine yoyote itakayoonekana inafaa.

Uwezo wa Bodi.

**13.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, usimamizi wa ujumla na miongozo ya kisera kuhusiana na utekelezaji wa kazi za Wakala utakuwa chini ya Bodi.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuajiri wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(b) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya muajiriwa wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni zake;

(c) kutaka taarifa au kuitisha kumbukumbu juu ya jambo lolote linalohusiana na uwezeshaji lililoamuliwa na Wakala; na

(d) kuingilia kati wakati wowote katika uendeshaji wa Mfuko ili kuepusha viashiria vinavyoweza kupelekea hasara au kushindwa kufanyika kwa marejesho.

Posho ya wajumbe

**14.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusika.

Mwenendo wa Bodi.

**15.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**16.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala atakayeteuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala.

Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

**17.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji, ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika Chuo kinachotambulika na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Idara, divisheni na vitengo.

**18.**-(1) Wakala unaweza kuanzisha idara, divisheni au vitengo kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wa idara watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni au vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Wafanyakazi wa Wakala.

**19.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Wakala watakaoajiriwa kwa kuzingatia vigezo na masharti kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake.

Kuanzishwa kwa Kamati ya Uongozi.

**20.**-(1) Kutakuwa na Kamati ya Uongozi ya Wakala ambayo itaundwa na:

(a) Mkurugenzi Mtendaji ambaye atakuwa Mwenyekiti; na

(b) Wakurugenzi wote wa Idara za Wakala.

(2) Kamati ya Uongozi inaweza kumualika mtu yeyote mtaalamu katika vikao vyake itakapoona inafaa.

Kazi za Kamati ya Uongozi.

**21.**-(1) Kamati ya Uongozi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuunganisha Wakala na sekta nyengine juu ya masuala yanayohusiana na uwezeshaji kiuchumi;

(b) kufanya uchambuzi yakinifu na kupendekeza juu ya ombi lililowasilishwa kwa Wakala na muombaji;

(c) kuushauri Wakala juu ya mjasiriamali au mfanyabiashara kufanya jambo mbadala;

(d) kupitia mpango kazi na bajeti ya Wakala;

(e) kushauri juu ya kuendeleza na kuimarisha shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(f) kuandaa ripoti na kuisambaza kwa wadau husika; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Bodi.

(2) Kamati ya Uongozi itakutana kila mwezi na itatoa taarifa kwa Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**22.** Kunaanzishwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.

Uendeshaji na usimamizi wa Mfuko.

**23.** Mfuko utaendeshwa na kusimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji chini ya maelekezo ya Bodi.

Vyanzo vya Mfuko.

**24.** Mtaji na gharama za uendeshaji wa Mfuko zitatokana na:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ruzuku halali, misaada, michango na fedha nyengine zitakazopokelewa na Mfuko kutoka katika vyanzo vyengine;

(c) mapato yatakayotokana au kupatikana na Mfuko kupitia mafunzo, ushauri elekezi na shughuli nyengine zozote zitakazofanywa na Mfuko;

(d) mkopo utakaopewa Wakala;

(e) fedha zitakazotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(f) mapato yanayotokana na huduma za kifedha zinazotolewa na Mfuko;

(g) ada na faini kutoka kwa mteja kama zitakavyoainishwa katika kanuni; na

(h) fedha nyengine zozote halali kutoka katika programu za uwezeshaji.

Malengo ya Mfuko.

**25.**-(1) Malengo ya Mfuko yatakuwa ni kuwezesha shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo yatajumuisha yafuatayo:

(a) kuweka mifumo imara ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa matumizi endelevu;

(b) kuimarisha huduma za mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara katika maeneo ya mjini na vijijini;

(c) kuweka mfumo wa mashirikiano na taasisi za kifedha kwa uendeshaji bora na kuifikia jamii kwa kiasi kikubwa;

(d) kusimamia kwa ufanisi urejeshaji wa mikopo iliyotolewa kwa mjasiriamali au mfanyabiashara kama itakavyoainishwa katika miongozo ya mikopo;

(e) kukusanya, kuchambua taarifa na kuandaa ripoti za utekelezaji; na

(f) kuchangia katika kuanzisha fursa za ajira.

(2) Katika kutekeleza kazi zake, Mfuko utazingatia makundi maalumu katika jamii.

Ukaguzi wa Mfuko.

**26.** Mfuko utakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine zozote zinazohusika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha.

**27.**-(1) Fedha na rasilimali za Wakala zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zinazopokelewa na Wakala kutokana na huduma zinazotolewa na Wakala;

(c) ruzuku halali, zawadi, msaada, michango, mikopo au uwekezaji kama Wakala utakavyoweza kupokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(d) fedha nyengine zozote ambazo zitawekwa au kupatikana kihalali na Wakala kutokana na utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

(2) Miamala yote ya fedha ya Wakala itafanywa na itaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine yoyote ya fedha.

Bajeti ya Wakala.

**28.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji, katika kila mwaka wa fedha, atawasilisha katika Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo juu ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi kwa ajili ya Wakala kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kutokana na majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Wakala itafanywa katika namna ile ile kama ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Wakala yataandaliwa kwa mujibu wa matakwa na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote inayoweza kutolewa na Serikali mara kwa mara.

(4) Mkurugenzi Mtendaji atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Wakala ni sahihi na yanaidhinishwa ipasavyo, na adhibiti ipasavyo mali na madeni ya Wakala.

Hesabu na ukaguzi.

**29.**-(1) Wakala utaweka na kutunza vitabu sahihi vya hesabu.

(2) Taarifa za fedha za mwaka zitakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine husika za fedha.

## SEHEMU YA SITA
## USAJILI WA MJASIRIAMALI NA MFANYABIASHARA

Maombi na taratibu za usajili.

**30.**-(1) Mjasiriamali au mfanyabiashara yeyote anayetaka kupata huduma za uwezeshaji kiuchumi kwa mujibu wa Sheria hii, anatakiwa kuomba kusajiliwa kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(2) Taratibu za maombi yatakayofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitakuwa kama itakavyoainishwa katika miongozo itakayotolewa na Wakala.

Daftari la kumbukumbu.

**31.**-(1) Wakala utaanzisha daftari la kumbukumbu za wajasiriamali na wafanyabiashara wote watakaosajiliwa na Wakala.

(2) Daftari la kumbukumbu litakuwa chini ya uangalizi wa Mkurugenzi Mtendaji.

Sifa za kusajiliwa.

**32.**-(1) Mjasiriamali au mfanyabiashara yeyote anayeomba kusajiliwa na Wakala anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) awe na Kitambulisho halali cha Mzanzibari Mkaazi;

(c) awe na leseni halali ya biashara;

(d) awe ana angalau umri wa miaka 18;

(e) awe anajihusisha na shughuli halali za kiuchumi zinazokubaliwa kwa mazingira ya Zanzibar;

(f) awe na akili timamu; na

(g) awe na uadilifu wa hali ya juu.

(2) Endapo mjasiriamali au mfanyabiashara ni kampuni au chama cha ushirika kitatakiwa kuwa na:

(a) cheti cha usajili cha kampuni ya ndani au cheti cha usajili wa chama cha ushirika kama itakavyokuwa;

(b) leseni halali ya biashara kama ipo; na

(c) kiwe kinajihusisha na shughuli halali za kiuchumi zinazokubaliwa kwa mazingira ya Zanzibar.

Cheti cha Usajili.

**33.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji baada ya kupokea maombi na kujiridhisha na maelezo yanayohitajika:

(a) atamsajili mjasiriamali au mfanyabiashara; na

(b) atatoa cheti cha usajili.

(2) Cheti cha usajili kinakuwa katika muundo na namna kama itakavyoainishwa katika miongozo.

Athari ya usajili.

**34.**-(1) Cheti cha usajili kilichotolewa chini ya Sheria hii, kitakuwa ni uthibitisho unaojitosheleza kwamba mjasiriamali au mfanyabiashara anajihusisha na shughuli za kiuchumi chini ya uangalizi wa Wakala.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mjasiriamali au mfanyabiashara atatakiwa kufuata masharti ya sheria nyengine husika.

Kufuta Cheti cha Usajili.

**35.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji wakati wowote, anaweza iwapo mjasiriamali au mfanyabiashara atashindwa:

(a) kufuata miongozo au maelekezo ya Wakala katika kutekeleza shughuli zake; au

(b) kufuata vigezo au masharti yoyote yaliyowekwa na Wakala katika usajili,

kutoa indhari ya kumtaka mjasiriamali au mfanyabiashara kufuata miongozo na maelekezo na masharti mengine yoyote yaliyowekwa na Wakala ndani ya muda kama utakavyoainishwa katika indhari.

(2) Mkurugenzi Mtendaji anaweza, endapo mjasiriamali au mfanyabiashara aliyesajiliwa atashindwa kufuata matakwa ya notisi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kufuta cheti cha usajili kinachohusiana na mjasiriamali au mfanyabiashara huyo.

Athari ya kufutwa kwa Cheti cha Usajili.

**36**-(1). Endapo Mkurugenzi Mtendaji amefuta cheti cha usajili, ndani ya siku kumi na nne, atamjuilisha mjasiriamali au mfanyabiashara maamuzi ya Wakala kuwa mjasiriamali au mfanyabishara huyo hatakuwa tena chini ya usimamizi wa Wakala na hatakuwa mnufaika wa huduma zinazotolewa na Wakala.

(2) Endapo mjasiriamali au mfanyabiashara amefutiwa cheti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatakiwa kulipa deni analodaiwa.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

**37.** -(1) Mtu ambaye:

(a) atatoa taarifa au maelezo akijua ni ya uongo;

(b) atashindwa kufuata amri au maelekezo yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria;

(c) amemzuia au amemshawishi vibaya mjumbe wa Bodi, Mkurugenzi Mtendaji au mfanyakazi wa Wakala katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii;

(d) ametumia fedha zilizotolewa au kupitia huduma za mikopo chini ya dhamana ya Mfuko kinyume na lengo lililokusudiwa;

(e) ameiba fedha zilizotolewa chini ya Sheria hii; au

(f) kwa uongo amejinasibisha, amewasilisha waraka wa kughushi, ametoa taarifa za kupotosha au amejipatia fedha au mali yoyote ya Mfuko kinyume na sheria,

ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Saba za Kitanzania kulingana na uzito wa kosa.

(2) Pamoja na faini iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu aliyetiwa hatiani atarejesha fedha alizokopeshwa.

Adhabu ya jumla.

**38.** Mtu aliyevunja sharti lolote chini ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyotolewa, ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Kitanzania.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Thamani ya Wadau wa Ndani na Jukumu la Ushirikishaji Jamii.

**39.** Wawekezaji wa ndani na wa kigeni watazingatia thamani ya ushiriki wa wadau wa ndani na jukumu la ushirikishaji jamii ili kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Rufaa.

**40.** Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukata rufaa kwa Waziri kwa mujibu wa taratibu kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Kanuni.

**41.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii, uendeshaji na usimamizi wa jumla wa Wakala.

Kufuta na kubakiza.

**42.**-(1) Tangazo la Kisheria Nam. 114 la 2015 la Kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar linafutwa itakapoanza kutumika Sheria hii.

(2) Aya ya (f) ya kifungu cha 26 cha Sheria ya Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar Nam. 2 ya 2018 inafutwa.

(3) Bila ya kujali masharti chini ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Tangazo la Kisheria Nam.114 la 2015 la Kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na aya ya (f) ya kifungu cha 26 cha Sheria ya Wakala wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar Nam. 2 ya 2018 litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

## MWENENDO WA BODI
**(Chini ya kifungu cha 15)**

---

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**1.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**2.**-(1) Bodi itakutana kila robo mwaka na inaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**3.** Akidi katika vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wake.

Maamuzi ya Bodi.

**4.** Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa maafikiano, ikiwa hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Taratibu za vikao.

**5.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake yenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha kamati za Bodi.

Mjumbe mualikwa.

**6.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe kuhudhuria katika majadiliano ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

**7.**-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada ya kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni wa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kamati za Bodi.

**8.** Bodi, kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zake, inaweza kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi mahsusi kama itakavyoona inafaa.

Kusita kuwa mjumbe.

**9.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) isipokuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji, ikiwa atasitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Wakala;

(e) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza; au

(f) kifo.

Kujiuzulu kwa Mjumbe wa Bodi.

**10.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa indhari ya maandishi kwa Mamlaka iliyomteua, na kuanzia siku iliyoainishwa kwenye indhari, au kama tarehe haikuainishwa, kuanzia tarehe iliyopolekewa notisi katika Mamlaka ya uteuzi, atasita kuwa Mjumbe.

(2) Mtu atakaposita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi vyovyote itakavyokuwa, kwa sababu yoyote, kabla ya kumaliza muda wake wa utumishi wa Bodi, Mamlaka ya uteuzi itamteua mtu mwengine kushikilia nafasi hiyo na mtu huyo aliyeteuliwa atashikilia ofisi kwa muda uliobakia wa mtangulizi wake.

Kukasimu kazi za Bodi.

**11.** -(1) Bodi inaweza, inapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mtendaji au kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 3 Machi, 2022.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***